JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

Website: www.uwembasec.com
E- mail ; headmaster@uwembasec.com
Kumb.. No. UWSS/JI/VOL 1/6
Mob. 0756213159(H/M) au 0754364441 (S/M)

SHULE YA SEKONDARI UWEMBA,
S. L. P. 241,
NJOMBE – TANZANIA.
25/11/2020

Kwa mawasiliano yote yanahusu mwanafunzi,
Wasiliana Kwa Namba:

1. Mwl. Clen Chaula 0758-703837
2. Mwl. Fred Salingo 0755-958103

Jina la Mwanafunzi

……..

S. L. P. .....

.....

YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UWEMBA, HALMASHAURI YA MJI NJOMBE, MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Uwemba ipo umbali wa Km 25 barabara ya kuelekea Wilaya ya Ludewa.

Usafiri wa basi kutoka Njombe unapatikana katika kituo cha Mabasi cha Njombe Mjini kwa nauli ya sh. 2000/= Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **11.01.2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **20/01/2021**. Baada ya hapo hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi asiyetaka kuleta mtoto shuleni kwa wakati.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

A; WAVULANA (HOSTELI)

1. Mashati 2 meupe mikono mifupi Tetron.
2. Suruali mbili (02) za shule rangi ya “Dark Blue” yenye mifuko miwili (02) mbele na mmoja (01) nyuma, upana miguuni inch 15-18, iwe na linda mbili (02) kila upande (dats), na yenye pindo chini/ mkunjo (turnup). (Ukishona model haitapokelewa)
3. Tshirt mbili za kijivu (aje nazo) mikono mifupi (yenye kola na iwe nzito)
4. Tracksuit ya rangi ya Dark blue /Nyeusi mstari mweupe pembeni (ukiweza njoo nazo 02)
5. Suruali nyeusi mbili za kazi za nje (isiyobana)
6. Viatu vyeusi-visigino vifupi jozi 2 vyenye kamba (Gidamu)
7. Nguo za ndani za kutosha angalau kuanzia 3 (chupi 3, vest nyeupe 3 aina ya spider)
8. Sweta ya rangi ya Blue yenye mshono wa V shingoni (jozi 02)
9. Raba za michezo, bukta mpya nyekundu na fulana nyekundu ya michezo.
10. Soksi nyeusi au khaki angalau kuanzia jozi 3 na kuendelea, mkanda mweusi na leso.

B; WASICHANA (HOSTELI)

1. Vigauni viwili “dark blue” vinavyogusa magoti (angalia mchoro), viwe na malinda
2. Suruali mbili za rangi ya” dark blue” (suruali za kubana hazitapokelewa), upana miguuni inatakiwa iwe na mkunjo (turnup), inchi 15-18.
3. Track suit ya rangi ya “dark blue”/ nyeusi mstari mweupe pembeni (ukiweza njoo nazo 02)
4. Tshirt mbili za kijivu (aje nazo) mikono mifupi (yenye kola na iwe nzito)
5. Sketi nyeusi mbili kwa ajili ya kazi (ndefu) zenye malinda
6. Viatu vyeusi-visigino vifupi jozi 2 vyenye kamba (Gidamu)
7. Soksi nyeupe angalau kuanzia jozi 03 na kuendelea na leso.
8. Nguo za ndani za kutosha angalau kuanzia 3 (chupi 3,taiti 3 na vest nyeupe 3 aina ya spider)
9. Kwa wanaovaa hijabu rangi ni nyeupe inayofunika kifua kama sare, na hijabu nyeusi kwa ajili ya kazi, Hijabu zisiwe na urembo wowote Jozi mbili (02) na kuendelea
10. Raba za michezo, bukta mpya nyekundu na fulana ya michezo nyekundu.
11. Sweta ya rangi ya Blue yenye mshono wa V shingoni (jozi 02)
12. Mashati 02 meupe mikono mifupi tetron

NB: Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na Raba au viatu vya mpira na soksi zake (rangi nyekundu)

-Pia vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa

2.2. Vifaa vya kulalia, chakula na usafi (wavulana na wasichana) Bweni na Kutwa

1. Kindoo cha lita 10 (kuogea), Taulo (Kanga kwa wasichana), Ndala, Kiwi nyeusi, Dawa ya meno na mswaki, Sabuni za kufulia na kuogea, na “toilet paper” (vitakaguliwa)
2. Sanduku imara la kutunzia vitu (tranka)
3. **Godoro Ft $2^{1/2}$ kwa 6 la QFLDodoma**
4. **Shuka 2 rangi ya pinki na blanketi nzito Uwemba kuna baridi**
5. **Vifaa vya kuleta, Wasichana na Wavulana**
   - Reki, Kwanja, Mopa, Jembe lenye mpini, Ufaguo mgumu (Hard Broom), Ufagio laini (Soft Broom), Chelewa na Panga.
6. **Sahani nyekundu 1, kikombe chekundu 1, bakuli nyekundu 1, na kijiko 1.**

2.3. Vifaa vya kujifunzia

1. Madaftari 20 (“Counter book” 10 quire 2 -3 za nukuu na daftari ndogo za kawaida 10 kwa ajili ya mazoezi)
2. Peni na kalamu za kutosha
3. Mkebe na rula ya futi moja
4. Ukiweza mnunulie mwanao vitabu vya masomo mbalimbali
5. Saa ya mkononi
6. Faili kwa ajili ya kutunzia mitihani

7. Kamusi ndogo ya kingereza kwa kingereza
8. Rimu 01 kwa kadri ya makubaliano ya kikao cha wazazi kila mwaka wa masomo.

2.4. Kwa wanafunzi wanaoishi Hosteli

1. Mahindi Kg 240 kwa mwaka (kilo 120 kwa muhula)
2. Maharage kg 60 kwa mwaka (kg 30 kwa muhula)
3. Mchele kilo 20 kwa mwaka (kilo 10 kwa muhula)
4. Fedha Tshs. 136,000/= kwa mwaka (68,000/= kwa muhula), Fedha hizi ni kwa ajili ya kununua sukari, chumvi, kuni, kusagia, umeme, kulipa wapishi na maji.
5. Mchango wa Matibabu Tshs. 5000/= (kwa mwaka) kwa ajili ya kununulia dawa na vifaa vya huduma ya kwanza na kumlipa nesi wa shule.
6. Kama kuna uwezekano unashauriwa umkatie mwanao Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu

NB Wanafunzi watakaopokelewa ni wale tu waliokamilisha michango yote, na michango itaanza kupokelewa kuanzia tarehe **28/12/2020 – 04/01/2021. Pia unapomleta mwanafunzi hakikisha una risiti ya benki (bank pay slip) na risiti ya chakula itakayomfanya mwanafunzi apokelewe kuishi Hosteli.**

Kama mzazi/mlezi ataona ni vema kumpa mtoto wake fedha za matumizi ni vizuri azitunze ofisi ya Uhasibu na mtoto atazichukua kadri ya uhitaji. Si vizuri mwanafunzi akakaa na fedha bwenini kwa vile hazitakuwa salama.

NB: Michango yote ya fedha ilipwe benki, Akaunti namba 60610003561, jina la akaunti ni UWEMBA SECONDARY SCHOOL

2.5. Uthibitisho wa Uraia

Mwanafunzi aje na kopi ya cheti cha kuzaliwa (**NI MUHIMU SANA**)

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na..25 ya mwaka 2978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu Nchini na Ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

A. Heshima kwa viongozi, Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
C. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
D. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
E. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
F. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
G. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
I. Kutunza mali za Umma

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

A. “Medical Examination form” ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
B. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
D.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. NI KOSA LA JINAI KUTOMLETA MTOTO SHULENI. ADHABU YAKE NI KUSHTAKIWA NA KUFUNGWA.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……..

CHENGULA A.A
MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI
UWEMBA
S.L.P 241
NJOMBE

FORM NO. 1

MAELEZO BINAFSI

1. Jina la mwanafunzi …….Kidato cha……mwaka…….
   Tarehe ya kuzaliwa…… Na. ya cheti cha kuzaliwa……
   Mahali ulipozaliwa (wilaya)……. Mkoa…….
   Dini yako……Dhehebu……
   Shule ya msingi uliyotoka……

2. BABA.
   i. Jina la baba……
   ii. Yu hai/ Amefariki……..
   iii. Anuani yake kama yu hai……...
   iv. Kazi yake……
   v. Ameajiriwa na idara / Amejiajiri……
   vi. Dini ya baba……
   vii. Simu ya mkononi ……

3. MAMA
   i. Jina la mama……
   ii. Yu hai/ Amefariki……
   iii. Auani yake kama yu hai……...
   iv. Kazi yake…….
   v. Ameajiriwa na Idara / Amejiajiri……
   vi. Dini ya mama…….
   vii. Simu ya mkononi ……

4. MLEZI
   i. Unaye mlezi (mlezi si mzazi lakini anakutunza na kukulipia gharama zote za mahitaji mbalimbali)
      Ndiyo/Hapana……
   ii. Kama jibu ni ndiyo
      (a) Jina la mlezi…….
      (b) Uhusiano na Mlezi(Mjomba,Kaka,Rafiki,Shangazi n.k)
   iii. Anuani ya mlezi……..
   iv. Dini ya mlezi……
   v. Kazi yake…….
   vi. Ameajiriwa na Idara / Amejiajiri……
   vii. Simu ya mkononi ……

5. Namba za simu za ndugu wengine wa karibu
   (i). Namba …… Uhusiano ……...…Jina……
   (ii). Namba …… Uhusiano ……..…Jina ……..……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MKOA WA NJOMBE

FORM NO. 2;

OFISI YA MKUU WA WILAYA,
WILAYA YA ……..
S. L. P. …….
…. ……

TAREHE:
……

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ……..
S. L. P. …….
……..

YAH: UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA.

Nathibitisha kuwa …… (Jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa.

Baba yake (jina kamili). ……

Amezaliwa katika Mkoa wa ……. Wilaya ya …….

Tarafa ya ……. Kata ya …….

Mama yake (Jina kamili) ……

Amezaliwa katika Mkoa wa ……..... Wilaya ya ……

Tarafa ya …… kata ya …… hapa nchini.

……

MKUU WA WILAYA

NB:- Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu, ikisha jazwa irudishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni. Kama una cheti cha kuzaliwa huhitaji kujaza fomu hii.

MEDICAL CERTIFICATE FORM.

FORM NO. 3:

To be completed by the medical officer in respect of form I entrance pupil's full

Name……Form/Class……
Age……..Years…… Sex…….
Blood count (Redand white)……...
Stool examination……..
Urine analysis……..……
T.B Test…….
Ears……
Chest……
Spleen……
Abdomen……
Sight
…….

ADDITIONAL INFORMATION. Physical defect or impairments infections chronic or family diseases
……
……
……
……
……
……
……
……
……

I certify that the above is fit/ unfit for admission into day/ boarding school

Signature……

Designation……

Station……

Date……

SHULE YA SEKONDARI UWEMBA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

A: MWANAFUNZI:

JINA LA MWANAFUNZI……..KIDATO .....MWAKA .....

ANUANI……..……..

TAREHE…….…….

Mimi……

Nimekubali/sijakubali kujiunga na jamii ya shule ya sekondari Uwemba. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtii na nitazingatia sheria/taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

Sahihi ya mwanafunzi…….Tarehe……..

……

B; MZAZI/MLEZI

Mimi…….Mzazi/Mlezi wa

……

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayohusu mtoto wangu.

Nimekubali/sijakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi pia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia.

Sahihi ya mzazi/mliezi……Tarehe……..

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/Kupata mimba/kusababisha mimba ndani na nje ya shule
9. Kuoa au Kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi, laini ya simu, chaja na vifaavyote vinavyo tumia umeme.
14. Kumiliki vitu hatarishi Mf. Nyundo, panga, mkasi, kisu, chupa n.k
15. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
16. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
17. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, viongozi na walezi
18. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI UWEMBA
S. L. P. 241.
NJOMBE

SHERIA ZA SHULE.

1. Msalimu Mtumishi yeyote wakati wowote unapoonana naye hasa kwa mara ya kwanza kwa heshima ya siku hiyo.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia (kunywa) kileo cha aina yoyote. Ni kosa pia kwa mwanafunzi kupika au kuuza kileo.
3. Mwanafunzi asimame wakati mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita au kuingia darasani
4. Mwanafunzi asivute au kuuza sigara.
5. Usizungumze na mwalimu au mtu anayekuzidi umri ukiwa umekaa, mikono ikiwa mifukoni ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kutembea usiku bila sababu yoyote hata kama atakuwa anakaa nyumbani kwa wazazi wake.
7. Mwanafunzi asihusishwe wala kufanya sherehe usiku.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kubishana na mwalimu au kiongozi yeyote. Uamuzi wa mwisho ni wa mwalimu. Malalamiko yeyote yapitie ngazi zilizowekwa kulingana na taratibu za shule.
9. Usipige kelele au kuleta ghasia sehemu zinazo hitaji ukimya. Kama darasani, bwenini.
10. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga au kupigana ndani au nje ya shule.
11. Daima uwe msafi kimwili na mavazi. Uwe na nywele fupi. Ndevu au masharubu haviruhusiwi shuleni.
12. Ni kosa kutumia lugha ya matusi.
13. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nywele za bandia wala kutumia rangi za kucha na midomo.
14. Haifai kwa mwanafunzi kuvaa nguo zinazoonyesha mwili, nguo fupi na viraka viraka. Mwanafunzi atunze heshima na adabu yake.
15. Ni marufuku kwa wanafunzi kujiunga na vilabu vya michezo nje ya shule.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki katika vigenge vya usengenyaji au kusema uongo.
17. Usifanye biashara ya aina yeyote shuleni.
18. usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa
19. Usikatae uteuzi wa kushiriki shughuli za michezo, uongozi n.k.
20. Usigune wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa tangazo kama kuna swali nyosha mkono, mikondo ya ustarabu ifuatwe
21. Usibandike au kuandika tangazo lolote lile bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.
22. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki aina yoyote ya nguo nje ya zile zilizoagizwa.
23. Huruhusiwi kuhubiri Dini, Siasa au jambo lolote katika mazingira ya shule.
    Sala zote zifanyike wakati uliopangwa na mahali panapohusika kwa mfano Kanisani au Msikitini.
24. **Mwanafuzi huruhusiwi kuwa na vitu vya thamani kama Simu, Camera, Ipad, Laptop, TV, Radio. Akikamatwa na vitu hivyo atarudishwa nyumbani kusubiri uamuzi wa bodi.**

Mimi ..... mwanafunzi
Niliyechaguliwa kuingia katika shule ya Uwemba nimesoma sheria za shule na kuzielewa
Naahidi kuwa nitazifuata zote ili niwe na maisha mazuri na ya raha shuleni.
Sahihi ya mwanafunzi ..... Tarehe .....
Sahihi ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....